# Twende Pamoja

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**

Hutolewa kila baada ya Miezi Mitatu Octoba-Disemba 2015 Toleo Na 003

**Ndani**

Madiwani wapitisha-Bajeti ya Halmashauri 2016/2017
Uk.6



Halmashauri ya Wilaya yapata Mkurugenzi Mpya.
Uk 3



Habari katika picha
Uk.7&8

# Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya Njombe lazinduliwa..........uk 5



*Wajumbe wa baraza la madiwani wa Halamshauri ya wilaya ya Njombe (wenye majoho) wakiwa katika picha ya pamoja na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe muda mfupi baada ya kuzinduliwa kwa baraza la madiwani.*

## Halmashauri yapiga marufuku usafirishaji wa mazao ya misitu Usiku.

Kufuatia baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kusafirisha mazao ya misitu usiku , Halmashauri ya wilaya ya Njombe imepiga marufuku usafirishaji wa mazao yatokanayo na misitu usiku.

Hivi karibuni imejitokeza tabia ya wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao ya misitu ikiwemo mbao, mkaa,nguzo na mirunda kusafirisha mazao hayo usiku kinyume na sheria, kanuni na miongozo inayoongoza uvunaji na biashara endelevu ya mazao

*Inaendelea Uk ....2*



**Mpango mkakati wa miaka mitano waanza kuandaliwa na Halmashauri.**
**Uk........3**

# Tahariri

Karibuni wasomaji wetu katika toleo lingine la *Twende Pamoja* ambalo ni gazeti linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe . Jarida hili hutolewa Kila baada ya miezi mitatu .

Dhima ya jarida hili mbali na kuhabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu pia ni kuwa nyenzo na daraja la kukuza maarifa na maendeleo katika Halmashauri .

Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha Jarida la *Twende Pamoja* linapatikana katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata ili kuwapa nafasi wananchi kusoma na kuelewa namna Halmashauri inavyotekeleza shughuli zake.

Tunaahidi kuendelea kutoa habari na makala ambazo zitakufanya uelewe namna sera zinavyotungwa, mipango inavyowekwa pamoja na utekelezaji wake unavyofanyika.

Tunatarajia matoleo yajayo yawe yamesheheni makala zenye kuelimisha na kuchochea maendeleo ya mtu mmoja mmoja, Kaya na Jamii kwa ujumla. Hii itakuwa nafasi nyingine ya kipekee ya kuweza kupata ujuzi na maarifa pasipo kuhitaji gharama.

Aidha tunakaribisha habari na makala mbalimbali kutoka kwenye Vijiji na Kata. Makala hizo zinaweza kuelezea jinsi utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zilivyofanyika katika Kijiji au Kata husika.

Tunakaribisha maoni na ushauri wa namna ya kuliboresha jarida hili kuweza kutimiza lengo la Halmashauri la kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji. Tunawatakia usomaji mzuri. Sasa “Twende Pamoja.

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

## Halmashauri yapiga Marufuku.....

*Inatoka Uk....01.*

Hivi karibuni imejitokeza tabia ya wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao ya misitu ikiwemo mbao, mkaa,nguzo na mirunda kusafirisha mazao hayo usiku kinyume na sheria, kanuni na miongozo inayoongoza uvunaji na biashara endelevu ya mazao ya misitu.

Kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 369 (1999), usafirishaji wa mazao ya misitu unatakiwa kufanyika kati ya saa12:00 asubuhi hadi saa 12:00 Jioni, hivyo usafirishaji wa mazao ya misitu usiku umepigwa marufuku.

Usafirishaji wa mazao ya misitu usiku umekuwa na athali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kutopata mapato stahiki yatakayosaidia kutekeleza miradi ya maendeleo..

Mfanyabiashara yoyote atakayekutwa akisafirisha mazao ya misitu usiku atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kufungwa jela miezi 6 au kutozwa faini ya shilingi 300,000 Serikali Kuu kwa kusafirisha mazao hayo usiku, Pamoja na faini ya kati ya shilingi 50,000 hadi 300,000 kwa Halmashauri.

Sambamba na hilo mfanyabiashara atatakiwa kulipia ushuru wa zao husika kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashuri ya wilaya ya Njombe.

Halmashauri inawataka wafanyabiashara wote kufuata sheria, kanuni na taratibu za usafirishaji wa mazao ya misitu ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

# Njombe yapata Mkurugenzi mpya

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imepata Mkurugenzi mpya baada ya Mkurugenzi wa awali Bw Paulo S. Malala kuhamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma.

Kufuatia uhamisho huo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe itakuwa ikiongozwa na Bi Hajjat Farida Mwasumilwe ambaye kabla ya kuhamishiwa Halmashauri hii alikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Upande wa Bw Malala ameiongoza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuanzia mwaka 2012 alipopokea uongozi kutoka kwa Bw Mohamed Juma Mkupete.

Bi Mwasumwile anakuwa Mkurugenzi wa tisa kuiongoza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tangu mwaka 1984 huku akiweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuiongoza Halmashauri ya wilaya ya njombe tangu 1984.

Mkurugenzi anayeshikiria rekodi ya kuongoza Halmashauri hii kwa kipindi kirefu ni Bw. Mohamed Juma Mkupete ambaye aliongoza kwa kipindi cha miaka 7 kuanzia mwaka 2006 hadi 2012 alipomwachia Bw Paulo S Malala.



*Mkurugenzi Mtendaji aliyehama Bw Paulo S Malala (Kushoto) akimkabishi nyaraka Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bi Hajatt Farida Mwasumilwe (kulia) Katika Hafla fupi ya Makabishiano iliyofanyika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*

## Mpango Mkakati waandaliwa.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe inaandaa mpango mkakati wa miaka mitano utakuwa dira na muelekeo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2021.

Kuandaliwa kwa mpango huu kunatokana na mpango wa awali uliandaliwa mwaka 2010/2011 kuisha kwa muda wake wa utekelezaji.

Ili kuhakikisha mpango Mkakati unaoandaliwa unakidhi kiu na matarajio ya wananchi Halmashauri imeshirikiana na wataalamu kutoka katika chuo cha Mipango Dodoma katika kuuandaa.

Aidha wadau mbalimbali wa Halmashauri watashirikishwa pindi mpango wa awali utakapotoka ili kuweza kuuboresha kabla ya mpango kamili kuzinduliwa hivi karibuni.

## Upasuaji wamama wajawazito kuanza Lupembe

Ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa wakazi wa Tarafa ya Lupembe wilayani Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inakusudia kuanza kutoa huduma ya upasuaji wa dharulakwa akina mama wajawazito katika Kituo cha Afya Lupembe.

Katika kufanikisha adhima hiyo Halmashauri inatarajia kukarabati jengo lililokuwa linatumika kwa ajili ya tohara ili huduma za upasuaji zianze kuanyika.

Tayari vifaa vya upasuaji vipo na mtaalamu mmoja kutoka Halmashauri amepelekwa katika hospitali ya Peramiho Mkoani Ruvuma kwa ajili ya kujifunza zaidi ili kuweza kuifanya kazi ya upasuaji kwa ufanisi pindi huduma itakapoanza hivi karibuni.

Kuanza kutolewa kwa huduma hii kutasaidia kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi ambavyo vilikuwa vinatokea wakati huduma hii haikuwepo.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambayo ina kata 12 na vijiji 45 inajumla ya vituo 27 vya kutolea huduma za afya. Kati ya hivyo kituo cha afya kipo kimoja.

# Madiwani wapitisha bajeti ya bilioni 23 kwa ajili ya shughuli za Halmashauri 2016/2017

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe limepitishwa rasimu ya mapendekezo ya bajeti ya Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Katika mapendekezo hayo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatarajia kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi 23.155 bilioni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Akisoma mapendekezo ya bajeti kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bi Waza Benjamini alisema kuwa katika kufanikisha bajeti, mapato ya ndani yanachangia kiasi cha Shilingi. 1.559 bilioni, fedha za ruzuku kutoka serikali kuu ni shilingi 19.19 bilioni na fedha za wafadhili kutoka nje ni shilingi 2.400 bilioni.

Kuhusu upande wa miradi ya maendeleo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatarajia kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi 5.396 bilioni kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato kutekeleza miradi yamaendeleo.

Fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo zinachangia kiasi cha shillingi 1.529 bilioni , fedha za nje ni shilingi 2.4 bilioni huku mchango wa halmashauri ukiwa ni milioni 566 na nguvu za wananchi ni milioni 500.

Bi Waza alivitaja vyanzo vya mapato kuwa ni ruzuku kutoka serikali kuu, michango ya jamii, Halmashauri kupitia mapato ya ndani pamoja na fedha za wafadhili. Katika bajeti hii Halmashauri imetenga milioni 55 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Matembwe ili kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Akizungumzia juu ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti inayoendelea ya mwaka 2015/2016, Bi waza alisema kuwa kuchelewa au kutotoka kabisa kwa fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe imekuwa changamoto kubwa pamoja na ubovu wa barabara hasa nyakati za masika.

Kuhusu utatuzi wa changamoto afisa mipango alisema Halmashauri imejipanga kuandika maandiko mbalimbali kwa ajili ya kukaribisha vitega uchumi pamoja na kuomba ufadhili ili kuongeza mapato ya ndani.

Aidha, alibainisha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iko katika hatua za mwisho kufunga mfumo wa mapato wa kielektoniki (iTax) ili kusaidia kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato.

Mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yameandaliwa kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo makubwa ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA), maelekezo yaliyotolewa katika ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015, Maelekezo ya Sekta za utekelezaji wa mpango wa matokeo makubwa sasa(Big results Now) pamoja na sera za kisekta.

Maeneo mengine yaliyozingatiwa katika uandaaji wa bajeti ni mipango shirikishi kwa kutumia dhana ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&)OD) iliyoibuliwa Kata zote pamoja na Mpango mkakati wa Halmashauri wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016




*Afisa Mipango wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bi. Waza Benjamini akiwasilisha mapango wa rasimu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 katika baraza maalumu la madiwani la kujadili bajeti.*

# Halmashauri ya Wilaya ya Njombe yazindua baraza laMadiwani.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imezindua baraza la madiwani ambalo litadumu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015-2020.

Baraza hilo lenye wajumbe 18 ambapo madiwani wa kuchaguliwa wapo 12, viti maalumu wako 5 na mbunge mmoja. Kuzinduliwa kwa baraza hilo kunafuatia kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwezi octaba mwaka 2015 ambao ulihusisha Rais, wabunge pamoja na madiwani.

Kuzinduliwa kwa baraza hilo kulikwenda sambamba na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri,Makamu mwenyekiti pamoja na wajumbe wa kamati mbalimbali za kudumu.

Katika uchaguzi wa mwenyekiti wa Halmashauri, Valentino Aidan Hongoli ambaye ni diwani wa Kata ya Ikuna alichaguliwa kushika nafasi ya mwenyeki wa Halmashauri huku nafasi ya makamu wa mwenyekiti ikienda kwa Vasco Marco Mgunda ambaye ni diwani wa Kata ya Mfriga.



*Madiwani wa Halmshauri ya wilaya ya Njombe wakiwa katika kikao cha baraza la madiwani baada ya kuzinduliwa kwa baraza hilo.*

Upande wa kamati za kudumu ambazo mwenyekiti wake hudumu kwa kipindi cha mwaka mmoja Julius Essau Salingwa alichaguliwa kuongoza kamati ya Uchumi na mazingira na Paulo Lutangilo Kinyamago alichaguliwa kuongoza kamati ya Huduma za jamii.

Sambamba na uchaguzi huo pia madiwani walikula kiapo kilichotolewa na hakimu huku kikishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa Mkoa na Wilaya ya Njombe.

Aidha, ili kuhakikisha madiwani wanatekeleza wajibu wao kwa uhakika, walipewa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Mafunzo hayo yalijikita kuwapa uwezo wa kutekeleza vizuri wajibu wao. Mafunzo hayo yalihusu Wajibu wa madiwani katika Halmashauri, Dhana ya utawala bora, Kanuni za kudumu za Halmashauri pamoja na ujazaji wa tamko la viongozi wa umma kuhusu mali na madeni.

# Madiwani watakiwa kuwatumikia wananchi

Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Sarah Dumba, amewataka madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kujikita katika kuwatumikia wananchi ili kuweza kukidhi matarajio ya wananchi kwa serikali ya awamu ya tano.

Bi Dumba aliyazungumza hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya madiwani yaliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao vizuri.

Akizungumza wakati wa ufunguzi huo Bi Dumba aliwataka madiwani waliochaguliwa kujikita katika kutatua kero za jamii ikiwa ni pamoja na usimamizi wa mapato pamoja na rasilimali za jamii na taifa kwa ujumla. “Matarajio ya wananchi kwa serikali ya awamu ya tano ni makubwa sana, wananchi watatupima kwa namna tutakavyokidhi kiu na matarajio yao naomba mkajikite katika kuwatumikia wananchi”.Alisema Bi Dumba.

“Naamini baraza hili limepata watu makini na mahili ambao wataiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupata maendeleo kwa kasi nzuri kwa sababu nyinyi ni wawakilishi wa wananchi, Mkishirikiana na wataalamu wa Halmashauri naamini kabisa Halmashauri hii itapiga hatua kubwa”.aliongeza Bi Dumba.

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo madiwani baada ya kuchaguliwa ili kuwawezesha kutekeleza wajibu wao kikamilifu. Mada walizofundishwa ni pamoja na wajibu na majukumu ya madiwani katika Halmashauri, dhana ya utawala bora, kanuni za kudumu za Halmashauri pamoja na namna ya ujazaji wa tamko la viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina jumla ya madiwani 17 na mbunge mmoja. Upande wa madiwani wakuchaguliwa wapo 12 na madiwani watano ni wa viti maalum.

# Namna elimumsingi bure inavyokuwa.

Kuelekea mwishoni mwa mwaka 2015 Serikali imetoa miongozo ya utekelezaji wa sera ya elimu ya mwaka 2015 sambamba na ufafanuzi wa dhana nzima ya elimumsingi bila malipo, hii ikiwa ni pamoja na wajibu wa wadau mbalimbali katika kufanikisha azma hiyo.

Elimumsingi bila malipo maana yake ni kwamba mwanafunzi atasoma (kuanzia elimu ya Awali hadi kidato cha nne) bila mzazi/mlezi kulipa ada wala michango ya fedha iliyokuwa ikitozwa shuleni kabla ya kutolewa kwa Waraka wa Elimu namba 5 na 6 wa mwaka 2015 uliofuta ada na michango hiyo.

Aidha, serikali imekwishapeleka fedha za uendeshaji wa shule katika shule zote za Serikali katika Wilaya zote ikiwemo Halmashauri Wilaya ya Njombe, hii ikiwa ni pamoja na maelekezo ya matumizi ya fedha hizo na hivyo hakuna mchango unaotakiwa kutolewa kwa kuwa ada na michango imefutwa.

Wanafunzi wanaokaa katika dahalia (hostel) hawatatakiwa kulipa mchango wowote kwa kuwa serikali inatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii ikiwa ni pamoja na matengenezo madogo madogo ambapo asilimia 10 ya fedha inayopelekwa shuleni itatumika kwa kazi hiyo ya matengenezo madogo madogo.

Uamuzi huu mzuri wa Serikali haujaondoa jukumu la Wazazi/walezi katika kuwahudumia watoto wao katika mambo yafuatayo;

Sare za shule na michezo.

Vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari na kalamu, Chakula kwa wanafunzi wa kutwa, Matibabu, Nauli ya kwenda na kurudi kwa wanaotumia usafiri na walioko shule za sekondari za bweni wakati wa likizo, Mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana kama vile magodoro, shuka na mito.



*Vifaa vya maabara katika shule ya Sekondari Sovi Kata ya Mtwango wilayani Njombe vinawawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo.*

Halmashauri ya wilaya ya Njombe inaamini kuwa ili dhana ya elimumsingi bila malipo iwe na tija wazazi/walezi wanapaswa kutekeleza wajibu wao ili kuwafanya watoto wao kukua kimwili, kiakili na kisaikolojia kwa kuwapatia mahitaji muhimu ya kibinadamu kama ambavyo wamekuwa wakifanya hapo awali.

Ni dhahiri kuwa pamoja na kutoa elimumsingi bila malipo, Serikali haiwezi kuchukua majukumu yanayopaswa kutekelezwa na wazazi/walezi.

Kwa vyovyote vile mtoto wa mwananchi yeyote hataondolewa shule eti kwa sababu mzazi/mlezi wake ameshindwa kutoa michango iliyokubaliwa na jamii inayohudumia shule husika.

Wazazi/walezi wanawajibika kutoa ushirikiano kwa watoto wao, shule, na serikali katika kuhakikisha kuwa mpango wa elimumsingi bila malipo unatekelezwa kwa ufanisi ili kufikia malengo ya upatikana wa elimu bora kwa manufaa ya watoto wao, Jamii na Taifa kwa ujumla.

Elimumsingi bila malipo ni utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ambayo inalenga kuwa ifikapo mwaka 2025 nchi iwe na uchumi wa kati. Lengo hili litafanikiwa kupitia sekta ya elimu na mafunzo ambapo inatarajia kuleta maendeleo ya haraka kwa kutumia rasilimaliwatu iliyoelimika.

Aidha, kwa kuwapunguzia mzigo wazazi/walezi kugharamia/kuchangia elimumsingi watapata muda zaidi wa kufanya shughuli za maendeleo na hivyo kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja naTaifa kwa ujumla hii ikiwa ni pamoja na kuwahudumia watoto wao kwa kuwapa mahitaji muhimu ya kibinadamu.

## Huduma za afya zaanza kutolewa Vijiji matiganjola na Ibiki.

Katika kuboresha huduma za afya kwenye jamii Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia Idara ya afya imeanzisha huduma za zahanati katika vijiji vya Matiganjola Kata ya Ikuna na Ibiki kata ya Igongolo wilayani hapa.

Kuanzishwa kwa huduma hizi kunafuatia kazi kubwa iliyofanywa na jamii ya kukarabati majengo na kutafuta nyumba za watumishi ambapo Halmashauri ilifanya ukaguzi na kujiridhisha kuwa zinaweza kuanza kutoa huduma ya afya huku mikakati ya ujenzi ikiendelea.

Tayari Halmashauri imechukua jukumu la kununua dawa ili huduma iendelee kutolewa katika zahanati hizo wakati maombi ya kibali cha dawa kwa ajili ya vituo hivi ili kupata ruzuku ya mgao wa dawa kama zahanati zingine za kiserikali yakisubiliwa kujibiwa. Sambamba na hilo tayari watumishi watatu wamepelekwa katika zahanati ya Matiganjola ambao ni afisa tabibu, muuguzi na mhudumu wa afya. Upande wa Ibiki tayari amepelekwa tabibu msaidizi na muuguzi yupo katika hatua ya kupelekwa.

Katika zahanati hizo huduma zimeanza kwa wagonjwa wa n je na huduma zingine zitaendelea kuongezwa mara baada ya kupata vifaa ikiwemo friji za kuhifadhia dawa na vitanda kwa ajili ya kuzalishia.

## Wanafunzi 612 wafanya mtihani wa kidato cha nne Njombe.

Jumla ya wanafunzi 612 wamefanya mtihani wa kumaliza kidato cha nne kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Katika mitihani hiyo iliyofanyika mwezi Novemba mwaka huu, Wasichana waliofanya mtihani walikuwa 398 na wavulana 214ambao ni sawa na asilimia 98.55 huku wanafunzi ambao hawakufanya mtihani wakiwa ni 11 wasichana wakiwa 7 na wavulana 4.

Wanafunzi waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu ni wale walioandikishwa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2012. Mwaka 2012 wanafunzi walioandikishwa kuingia kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe walikuwa 1645 wasichana wakiwa 927 na wavulana 715.


Aidha, kati ya wafunzi 1645 walioandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2012 wanafunzi 505 hawakufika kidato cha nne mwaka 2015 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo utoro, ugonjwa, vifo pamoja na kukariri darasa kutoka na kufeli mtihani wa kidato cha pili.

Katika wanafunzi 505 walioshindwa kumaliza mtihani wa kidato cha nne mwaka huu wasichana ni 329 na wavulana ni 176 na hakuna mwanafunzi yoyote aliyeshindwa kumaliza mtihani ya kidato cha nne kutokana na mimba.

Ili kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaokariri madarasa inapungua Halmashauri ya wilaya ya Njombe kupitia Idara ya Elimu ya Sekondari imeweka mikakati mbalimbali kufanikisha suala hilo.

Mikakati hiyo ni pamoja na Kuhakikisha shule zinatoa chakula cha mchana ili kuwapa wanafunzi muda mwingi wa kujifunza, kuwapa masomo rekebishi pamoja na kuwapa ushauri ili kuwajengea mazingira mazuri ya kijifunza.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inajumla ya Shule 12 ambapo jumla ya Shule 10 zilifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu na mtihani huo umefanyika kwa njia ya amani na utulivu na hakukuwa na tukio lolote la udanganyifu lililotokea.




*Wanafunzi wa shule ya Sekondari Sovi wakiwa katika mafunzo kwa vitendo kabla ya mtihani wa Taifa*

# TANGAZO

Halmashauri ya wilaya ya Njombe imefanya marekebisho ya sheria ndogo zinazohusu Ada na ushuru wa mazao, bidhaa na huduma mbalimbali ambapo sheria ndogo hizo zimeshatolewa katika gazeti la Serikali kwa **Tangazo la serikali Na. 471 la 23.10.2015.**

Kwa mujibu wa tangazo la serikali Na 471 (2015)

i. Kila msafilishaji wa mazao ya misitu atatakiwa kulipa tozo asilimia ishirini (20%) juu ya ada ya usafirishaji (Transist Pass-TP) wa mazao ya misitu. Kwa tafsiri hiyo,

| S/Na | Ujazo wamzigo katika Gari | Tozo la 20 Halmashauri(HW5) |
|---|---|---|
| 1 | Zaidi ya Tani 7 | 3000/= |
| 2 | Chini ya Tani 7 | 1500/= |

ii. Kila mfanyabiashara wa mazao ya misitu atatakiwa kulipa tozo ya asilimia kumi (10) juu ya ada ya Usajili ya wafanyabiashara wa Mazao ya Misitu na wenye Viwanda vya kuchakata mazao ya misitu . Viwango vya tozo hizi vimeambatanishwa hapa chini. Tozo hii haitawahusu wafanyabiashara wa mazao ya misitu waliokwisha sajiriwa kabla ya Tangazo la Serikali Na 471 la Octoba 23,2015

Tozo hizi zitawahusu wafanyabiashara wote wanaofanyia kazi katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

**Atakayekiuka agizo hili atatozwa faini ya kiasi cha shilingi elfu hamsini (Tsh 50,000) na Au kifungo cha miezi kumi na mbili(12)**

MCHANGANUO WA VIWANGO VYA TOZO ZA ADA YA USAJILI WA WAFANYABIASHARA WANAOJISHUGHULISHA NA UCHAKATAJI AU BIASHARA YA MAZAO YA MAZAO YA MISITU KWA ENEO HUSIKA KWA KILA MWAKA.

| S/Na | AINA YA ZAO LA MISITU/ BIASHARA | ADA YA HATI YA USAJILI (REGISTRATION) INAYOLIPWA SERIKALI KUU (ERV) TSHS | TOZO LA 10% LA ADA YA USAJILI (TSHS) HW5 INALIPWA HALMASHAURI. |
|---|---|---|---|
| 1 | Biashara ya Mbao (Timber) | 256,000 | 25,600 |
| 2 | Biashara ya Magogo (Logs) | 256,000 | 25,600 |
| 3 | Biashara ya Nguzo (Poles) | 256,000 | 25,600 |
| 4 | Biashara ya Miti (Trees) | 270,000 | 27,000 |
| 5 | mashine za kuchana Mbao (Sawmill) 5000m3 per year | 512,000 | 51,000 |
| 6 | Mashine za kuchana Mbao (sawmill) 5001-10,000m3 per year | 1,000,000 | 100,000 |
| 7 | Kiwanda cha kutengeneza Chipboard (ChipboardMill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 8 | Kiwanda cha kutengeneza Hardboard (Hardboard Mill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 9 | Kiwanda cha kutengeneza Plywood (Plywood mill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 10 | Kiwanda cha kutengeneza Karatasi | 2,000,000 | 200,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Kiwanda cha kutengeneza Viberiti (Match Box Factory) | 1,000,000 | 100,000 |
| 12 | Kiwanda cha kutibu Mazao ya Misitu (Nguzo,Mbao nk) Impregnation Plant | 512,000 | 51,200 |
| 13 | Duka la Vinyago na Mapambo yatokan-ayo na Mazao ya Misitu (Curio Shops-Forestry Products) | 256,000 | 25,600 |
| 14 | Watoaji wa mazao ya Misitu nje ( Export-ers of Forestry Products) | 512,000 | 51,200 |
| 15 | Waingizaji wa mazao ya Misitu ndani ya Nchi (Importers of Forestry Products) | 512,200 | 51,200 |
| 16 | Biashara ya Mkaa (Charcoal) | 256,000 | 51,200 |
| 17 | Biashara ya Kuni (Firewood) | 256,000 | 51,200 |
| 18 | Duka la Samani ( Furniture Mart) Kubwa | 256,000 | 51,200 |
| 19 | Duka la Samani (Furniture Mart ) Ndogo | 256,000 | 51,200 |
| 20 | Kiwanda cha kuchakata Miti au Mbao (Wood Works Factory) Mashine za kuke-reza n.k Kubwa | 384,000 | 38,400 |
| 21 | Kiwanda cha kuchakata miti au mbao (Wood Works Factory) Mashine za Kuke-reza n.k Ndogo | 150,000 | 15,000 |
| 22 | Fundi Seremala (Carpentry) | 50,000 | 15,000 |
| 23 | Biashara ya mazao mengine ya Misitu | 130,000 | 13,000 |

**N:B Utekelezaji wa Agizo hili unaanza mara moja.**

Limetolewa na
Hajjat Farida A Mwasumwilwe
**Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.**

## KUTOKA MAKTABA





*Kushoto wataalamu wa Halmashauri na madiwani wakikagua ujenzi wa zahanati na kulia ni madiwani kutoka Halmashauri za Njombe, Wanging'ombe na Mji Makambako wakiwa katika picha ya pamoja na mkuu wa mkoa wa Njombe (katika) Aseri Msangi baada ya kusaini taarifa ya makabidhiano ya mgawanyo wa Halmashauri.Picha hizi zilipigwa mwaka 2013.*

# Njombe watekeleza kwa vitendo agizo la Rais Magufuli

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imetekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr John P Magufuli la kuitumia tarehe 9 Disemba 2015 kufanya usafi wa mazingira ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya uhuru wa Tanganyika.

Katika kutekeleza agizo hilo kila Kata imefanya shughuli za usafi wa mazingira katika taasisi za umma zikiwemo zahanati, shule za msingi na sekondari, maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya wazi pamoja na kwenye kaya.

Uzinduzi wa maadhimisho ya usafi wa mazingira ulifanywa na mbunge wa jimbo la Lupembe ambalo liko katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bw Joram Ismael Hongoli kwa kufanya usafi katika ofisi za Halmashauri hiyo zilizopo mjini Njombe.

Kiwilaya kilele cha maadhimisho ya uhuru kilifanyika katika Tarafa ya Lupembe ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Bi Sarah Dumba ambaye ambaye aliwaongoza viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Njombe pamoja na wananchi kufanya usafi katika kituo cha afya Lupembe.

Akizungumza na viongozi pamoja na wananchi walioshiriki zoezi hilo Bi Dumba aliwataka viongozi na wananchi kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya uhuru mwaka huu inayosema Tanzania bila kipindupindu inawezekana, zuia maambukizi mapya kwa kuzingatia usafi.

"Tunatakiwa kutekeleza kwa vitendo kauli hii kwa kuhakikisha kuwa sisi pamoja na jamii inayotuzunguka tunadumisha hali ya usafi wa mazingira, Hii itawezekana tu kama sisi viongozi tutakuwa makini katika kusimamia, kuhamasisha na kufuatilia kwa ukaribu mkubwa utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo tunayoyasimamia." Alisema bi Dumba.

Amewataka wananchi kuendelea na suala la usafi wa mazingira kwa muda wote badala ya kusubili maadhimisho pekee.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bw Paulo Malala, alimuhakikishia mkuu wa Wilaya ya Njombe kuwa kipindupindi hakiwezi kutokea katika Halmashauri hiyo.

Alisema kuwa Halmashauri ya Njombe imejipanga vizuri katika suala la usafi wa mazingira kutokana na kuwepo kwa kampeni ya afya na usafi wa mazingira ambapo Halmashauri ya wilaya ya Njombe ni miongoni mwa Halmashauri zinazotekeleza kampeni huyo.

Bw Malala alisema kupitia kampeni hiyoelimu juu ya usafi wa mazingira imekuwa ikitolewa jambo lililochangia wananchi kuwa na mwamko mkubwa katika ujenzi wa vyoo bora pamoja na msuala ya usafi wa mazingira.

Bw malala aliongeza kuwa sambamba na mikakati ya kuhakikisha kuwa kila Kaya inakuwa na choo bora na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, inatoe elimu kwa wananchi ili waweze kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vyoo vinakuwa safi wakati wote na kuhimiza unawaji wa mikono kwa maji safi na sabuni ili kuondokana na ugonjwa wa kipindupindu.



Mkuu wa wilaya ya Njombe Bi Sara Dumba akipanda maua katika kituo cha afya Lupembe ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya uhuru wa Tanzania Bara.



Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Njombe (sasa Kasuru) akikwatua uwanja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Uhuru



*Diwani wa Kata ya Kidegembye Julius Salingwa (kushoto) akisaini hati ya kiapo mbele ya hakimu John Paulo Kapokolo (Kulia) wakati wa kuzindua baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*



*Wataalamu wa Halamshauri ya Wilaya ya Njombe wakiwa katika mafunzo ya kuandaa mpango mkakati wa Halmashauri katika shule ya sekondari Njombe.*



*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Sara Dumba akipanda maua katika kituo cha afya Lupembe ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya uhuru ambayo iliadhimishwa kiwilaya kwa kufanya usafi kituoni hapo.*




*Mbunge wa jimbo la Lupembe Joram Hongoli akiongea wakati wa kuzindua baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Kushoto ni afisa wa serikali za mitaa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Njombe Bw Joseph Makinga.*



*Mkurugenzi mtendaji aliyehamishwa Bw. Paulo Malala (kulia) akimkabidhi hati na nyaraka Mkurugenzi mpya Bi Hajatt Farida Mwasumwile (kulia) katika dhifa fupi ya makabidhiano ya ofisi Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*



*Mkurugenzi mtendaji anayeondoka Bw Paulo Malala (kushoto) akiwa na Mkurugenzi mpya Bi Hajatt Farida Mwasumilwe(katika)wakisaini hati za makabidhiano wakishuhudiwa na mwenyekiti wa Halmashauri Bw Valentino Hongoli (kulia)*




*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Mh. Valentino Hongoli akizungumza katika kikao cha baraza la madiwani mara baada ya kuchaguliwa kuwa mwenyekiti.*



*Madiwani wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakifuatilia kwa makini uwasilishwaji wa makisio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017.*




*Mbunge wa jimbo la Lupembe Bw. Joram Hongoli lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe akifyeka nyasi kuzinduzi siku ya kufanya usafi katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe..*



*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Sara Dumba akipanda maua baada ya kufanya usafi katika Kituo cha afya Lupembe ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Uhuru kiwilaya iliyofanyika Tarafa ya Lupembe.*





*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi. Sara Dumba akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha wadau wa kilimo cha zao la mahindi kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya njombe Hajjat Farida Mwasumilwe (kushoto) akisisitiza jambo kabla ya ufunguzi wa baraza la madiwani*